EDWARD MORINGE SOKOINE:
FIKRA ZAKE JUU YA MAENDELEO

NA

ISSA G. SHIVJI
PROFESA
CHUO KIKUU CHA DAR ES ALAAM
ishivji@ud.co.tz

Aprili 7, 2004, Ukumbi wa Karimjee

Kwanza kabisa ningependa kuishukuru familia ya marehemu EDWARD MORINGE SOKOINE kutupatia nafasi hii ya kutathmini mchango wa kiongozi wa kitaifa, hasa kwa sababu, Sokoine ni kiongozi mmojawapo ambaye alikuwa na msimamo wa kipekee katika historia ya viongozi wetu wa kitaifa. Kwa upande wangu, napenda kuyachambua mawazo, fikra na mwelekeo wake juu ya suala la maendeleo ili kuuainisha msimamo wake. Awali kabisa ninatoa hoja kwamba Edward Sokoine alikuwa na msimamo maalum juu ya maendeleo katika nchi yetu. Msimamo huo, ambao nitauainisha kwa jina baadaye, ulikuwa unajitokeza katika jinsi alivyokuwa ana angalia masuala mbalimbali ya kijamii kama utamaduni, kilimo, uwekezaji, maendeleo vijijini, n.k.

Kutokana na hotuba zake mbalimbali tunaweza tukasema kwamba Sokoine alikuwa anasisitiza sana mambo yafuatayo: Moja, **Uhuru wa Kitaifa** [National Independence]; pili, **Kujitosheleza kwa chakula** [food self-sufficiency]; tatu, **soko la kitaifa** [national market]; nne, **uwekezaji katika kilimo na ufugaji** na tano **'mapinduzi vijijini'**. Kwa muhtasari tu, nitagusia maeneo haya matano kwa kutoa ufafanuzi pamoja na kunukuu maneno yake mwenyewe juu ya mambo haya.

I. UHURU WA KITAIFA

Msimamo wa Marehemu juu ya umuhimu wa kulinda na kukuuza uhuru wetu kama nchi na taifa ulikuwa wazi na imara. Na alidiriki kutoa masimamo huo bila kulegalega wala kutafuna maneno. Bila uhuru wa kitaifa, Sokoine aliamini, huwezi kuwa na maendeleo, hasa maendeleo yanayoheshimu utu wako kama binadamu. Aliwalaani sana, tena bila kusita, wale ambao **"wanaweza wakathubutu hata kuuza uhuru wa nchi zao ili waendelee kuishi lakini kuishi kitumwa."**

Tunaweza tukatambua vipengele vinne, ambavyo kwa pamoja, vinadhihirishi msimamo huo wa Sokoine. Kwanza **UTAMADUNI, MILA NA DESTURI**; pili, ni **UZALENDO**, tatu ni **KUJITEGEMEA KITAIFA**; na nne ni **KUTUMIA UTAALAM WA KITAIFA.**

Sokoine hakuamini kwamba mila na desturi zetu zote ni nzuri isipokuwa alilaani sana kuiiga mila na desturi za nje, hususun za jamii za Ulaya na Marekani, bila kujali uzuri au ubaya wake. Jambo hili alisisitiza katika hotuba yake muhimu aliyoitoa mwezi wa Oktoba, 1982, akiwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Arusha. Akasema:

> Ndugu Mwenyekiti, jambo la tano ambalo ningependa nilitaje, hili nalo ni la msingi vile vile, ningewaomba Wajumbe tusitupilie mila zetu nzuri mbali. … utamaduni wetu na mila zetu umeingiliwa mno na mila na tabia za kigeni za kuwa na tamaa ya vitu, hasa visivyosaidia katika maisha.

Kwa mantiki hiyohiyo, pia alisisitiza **UZALENDO** kwa maana ya upendo wa nchi yako na watu wake. Kwake yeye, uzalendo ulikuwa sifa mojawapo ya kiongozi bora. **"Kwa hivyo"**, akasema Sokoine, **"suala la uzalendo … lazima tulitumie katika kuwafikiria viongozi wenye masimamo wanaotaka kuchaguliwa Kitaifa ili kulisaidia Taifa letu**

katika kipindi hiki kigumu." Kwa Sokoine, uongozi sio dhamana tu bali ni kujitolea na kuwa mstari wa mbele katika vita vya kuwakomboa kimandeleo waliowengi, hususun, wanakijiji. Akiwahotubia Madisi, akasema:

> Nasikia baadhi ya viongozi huko mikoani wanagombania nyumba na magari. Mambo haya sio muhimu. Viongozi watafanya vizuri wakigombea juu ya maendeleo ya wanavijiji. Huo ni ugomvi mtakatifu, sawa na mwananchi anayeiba mbolea, na kutumia vizuri katika shamba lake.

Hakuna jambo ambalo Sokoine alikuwa anasistiza kila mara isipokuwa lile la **KUJITEGEMEA KITAIFA.** Kwake yeye, kujitegemea ilikuwa kama imani ambayo huwezi kuiacha bila kupoteza uhuru na utu wako. Kama tunavyofahamu 'Ujamaa na Kujitegemea' ilikuwa sera ya Chama na Serikali nyakati zile. Kwa hivyo, kama ilivyo desturi ya viongozi wengi, 'Ujamaa na Kujitegemea' ilikuwa inaimbwa hata kama mwimbaji hakuwa na chembe cha imani na sera hiyo. Wengine walidhoofisha tu maana ya Kujitegemea kwa kusema kila kaaya, kila kijiji, kila wilaya, kila mkoa n.k. lazima ujitegemea. Kwa Sokoine, kujitegemea maana yake ilikuwa kujitegemea kitaifa sio kikaaya au kiwilaya. Hakuna sababu, Sokoine kasema, kwa mikoa michache kuji*specialize* katika, kwa mfano, kulima chakula ili kutosheleza mahitaji ya nchi nzima. Ndio maana, Sokoine aliondoa maramoja vikwazo wa kusafirisha chakula kutoka mkoa moja kwenda mkoa mwingine. Kwa maana hiyo ya kujitegemea, alikuwa anapenda sana kurudiarudia maneno ya kwamba lazima **"kusimama kwa miguu yetu wenyewe"**.

Na kwa mantiki hiyo Sokoine alikuwa kiongozi mmojawapo ambaye alichukia sana kuombaomba chakula kutoka nchi za nje. Bila kujitegemea kwa chakula, tutaendelea kuwa wategemezi na kwa hiyo tutapoteza heshima, utu na uhuru wetu mbele ya jamii za

kimataifa, alionya Sokoine. Nainukuu tena hotuba yake ya Oktoba. Akimambia Mwenyekiti, bila shaka Mwalimu Nyerere, akasema:

> Jana ulitumia maneno ya kusema, "mwalimu mmoja wa zamani aliwaambia wanafuzi wake kwamba ukweli utawakomboa." Nafikiri kwa hivyo ungeweza ukatuambia kwamba kujitosheleza kwa chakula kwa Watanzania, vile vile kutatukomboa na kulinda uhuru wetu.

Jambo jingine alilolisisitiza sana katika dhana hii ya kujitegemea, Sokoine alitaja kuwategemea wataalam na wasomi wetu wenyewe badala ya kuwaabudu wale kutoka nchi za kigeni. Hilo ni la kipekee kwa sababu, kama tunavyofahamu, viongozi wetu wengi hupuuza wasomi na wataalam wetu ama kwa kuwaonea uvivu au kwa sababu ya shinikizo la wafadhili. Yeye alitambua kwa dhati kabisa umuhimu wa kuwa na imani na wataalam wetu na pia umuhimu wa utafiti wa kisomi kabla ya kufanya maamuzi ya kisera na kisiasa. Kama mhadhiri kijana, ninakumbuka Sokoine alitoa hotuba moja mnamo miaka ya '80 ambayo ilitufurahisha sana kwa kutambua nafasi ya wasomi katika maendeleo ya nchi. Sinabudi nimnukuu:

> Kwa mujibu wa nadharia kuhusu maendeleo, nchi yoyote haiwezi ikaendelea bila kuwa na mijadala juu ya mielekeo mbalimbali ya maendeleo. Jukumu mojawapo la wasomi wa Kitanzania ni kuchochea na kuongoza mijadala hii… .

II. Ujumuisho

Tukijumuisha mawazo mbalimbali ya Edward Moringe Sokoine, ambayo nimegusia kidogo, ningependa kutoa hoja kwamba misingi mikuu ya msimamo wa Sokoine ilikuwa Uhuru wa Kitaifa kwa kukiegemea kwenye uchumi wa kujitegemea, yaani, kwa maneno yake, **"kusimama kwa miguu yetu wenyewe"**. Kwa maana hiyo, Sokoine alipinga kabisa uchumi tegemezi au viongozi vichwara. Msimamo wake ulikuwa dhidi ya

Ubeberu na Uchwara, yaani, *anti-imperialist* na *anti-comprador*. Alilaani sana viongozi, wakiwa wa Tanzania au nchi zingine za Afrika, ambao walikuwa tayari kuuza uhuru wa nchi yao ili wapewe visenti vya misaada. Kwa maneno yake mwenyewe, [nanukuu]:

> Sijui kama nitaeleweka vizuri, Ndugu Mwenyekiti, lakini mpaka sasa nchi zilizo nyingi za dunia ya tatu hasa katika Africa tulio na matatizo ya kiuchumi tuna uhuru wa bendera hatuna uhuru wa kiuchumi na ndio huu tunaopigania. Lakini baadhi yetu ni lazima niwataje wameanza kuuza uhuru wa nchi zao, kutoa maeneo ya Kijeshi kwa nchi zilizoendelea ili mradi wawe na hakika wanaendelea kupata misaada. Hilo ndilo nasema ni suala la kuuza uhuru wa nchi.

Na aliendelea kuwalaani "viongozi" ambao **"wanaweza wakatumiwa na Mataifa ya nje au hata vibaraka wa ndani kwa lengo la kubadili siasa yetu au kuidhoofisha."** Alipokuwa anazungumza mambo haya, bila shaka, Sokoine alikuwa hawazii nchi yake, isipokuwa sina uhakika angesema nini katika enzi hizi za utandawazi!!

III. Msimamo wa Sokoine

Kwa kukosa muda siwezi nikaeleza kwa ufasaha zaidi mawazo mengine ya Sokoine. Isipokuwa nitaje harakaharaka tu kwamba Sokoine alisisitiza **kutosheleza kwa chakula**, **soko la kitaifa** na **uwekezaji katika kilimo na ufugaji.** Kwake yeye, mahala na chimbuko la maendeleo lilikuwa kijiji. Wakati viongozi wenzake wakizungumzia Vijiji vya Ujamaa na Vijiji vya Maendeleo, Sokoine alikuwa ana himiza dhana ya **'Mapinduzi Vijijini'**. Kwake yeye kijiji hakikuwa tu "kikapu" cha kupokea maagizo au maendeleo kutoka juu au kituo cha kutoa huduma za kijamii, bali kijiji ni chimbuko la kuleta mapinduzi ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa. Akasema:

> Badala ya kuzalisha malaki ya wataalam tuwageuze wakulima na wafugaji wawe ndio wataalam wenyewe.

Na akaongeza:

> Elimu inayohitajiwa vijijini kwanza kabisa ni kuimarisha na kuinua ustaarabu ili watu wasiridhike na maisha duni, elimu ya aina ya pili ni ufundi, na ya tatu ni elimu ya kuelewe mazingira ya kijamii ili watu waelewe nafasi yao katika jamii.

Pamoja na ukweli kwamba fikra za Sokoine juu ya suala zima la mtaji kama kichocheo cha maendeleo haziku kamilika, tunaweza tukasema kwamba, kwa jumla, yeye alikuwa anapendelea mtaji wa ndani, na sio wa nje, na aliona kilimo ndio chimbuko la kuzalisha na kulimbikiza mtaji. Kwa hivyo, sidhani kwamba Sokoine alikuwa anapinga mfumo wa kibepari kwa maana ya mali binafsi (*private property*) bali alitofautisha kati ya **Ubepari wa Kitaifa** (“national capitalism”) na **ubepari-uchwara** (“compradorial capitalism”) au **ubepari-tegemezi** (“dependent capitalism”.).

[Ili nisieleweke vibaya, ningependa kuweka wazi kwamba dhana ya ubepari wa kitaifa haina uhusiano wowote na ubepari wa ki-uzawa (“indigenous capitalism”.) kwa sababu ni wazi kwamba wazawa wanaweza wakawa vibaraka na kwa hivyo kuukuuza ubepari-uchwara na pia inawezekana kabisa wazalendo wote sio wazawa lakini hutetea uchumi huru kwa lengo la kujenga ubepari wa kitaifa. Kwa kifupi, unaweza ukawa mzawa bila kuwa mzalendo na unaweza ukawa mzalendo bila kuwa mzawa!]

Mwishowe, Ndugu Mwenyekiti, ningependa kutoa hoja kwamba Sokoine alikuwa kiongozi pekee ambaye tunaweza tukamuita mtetezi wa Ubepari wa Kitaifa. Hata Mwalimu Nyerere akiwa rais sidhani kwamba alitofautisha kati ya Ubepari wa Kitaifa na Ubepari-Uchwara isipokuwa baada ya kung’atuka. Mnamo nwishoni mwa miaka ya 80, ninakumbuka Mwalimu alitoa hotuba moja kwa viongozi wa serikali, chama na

mashirika ya umma. Kwa mara ya kwanza alitofoautisha kati ya ubepari wa kitaifa na ubepari-uchwara. Ninapenda kunukuu maneno yafuatayo ya Mwalimu mara kwa mara kwa sababu ya busara na ukweli wake, hata katika milenia hii ya utandawazi na sayansi na teknologia: :

> Ndugu Mengi mkipenda msipende mtatuuzia tu Coca-cola basi Coca-cola inauzwa tu. Sasa uchumi wetu basi ni uchumi tegemezi. ... Hili tatizo letu kubwa la msingi. ...
>
> Kwa hiyo tunajivunia ule ugonjwa... tunajivunia ule ugonjwa wala hatuuonei haya ... unaparedi silaha za wakubwa, unaparedi madege ya wakubwa, unaparedi bidhaa za wakubwa, unaparedi Macoca cola ya wakubwa na unajivunia tu unasema sisi tumeendelea. Ukimwambia umeendelea kwanini, anakwambia njoo uone barabara yetu.

Naam, siku hizi tunaparedi utandawazi wa wakubwa na tunasema haya ni maendeleo!

Ni sawa na inzi aliyenaswa na utandobui akijigamba kwamba ana fursa sawa na buibui!

Ndugu Mwenyekiti na Waheshimiwa Washiriki: Sinahaja ya kusisitiza kwamba Edward Moringe Sokoine alikuwa na sifa za kipekee katika viongozi wetu tangu Uhuru. Ni kati ya viongozi wachache waliyojijengea upendo na umaarufu katika nafsi ya Taifa kutokana na uhuru wao wa mawazo na utetezi wa wanyonge bila kuwaegemea, au kujipendekeza kwa Wakuu.

Ninashukuru familia ya marehemu Sokoine kunipa nafasi hii ya kutoa maoni yangu kuhusu fikra za Kiongozi huyu ambaye historia itamkumbuka hata kama viongozi wenzake na waliomfuata wangependa asahaulike!

Asante sana.

****